

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegrams "AFYA", DODOMA  
Nambari ya simu: +255-026-2323267/2351196  
Nukushi Na: +255-22-213806



Mji wa Serikali - Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S. L. P 743,  
**40478 DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI**

**UFAFANUZI KUHUSU UPIMAJI WA VIRUSI VINAVYOSABABISHA UGONJWA WA COVID-19 KWA WASAFIRI WANAOINGIA NCHINI.**

Dodoma, Jumanne Mei 18, 2021.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeendelea kuchukua hatua na tahadhari dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 ulioikumba dunia ambapo, kumejitokeza kuriptiwa kwa anuai mpya ya virusi vya ugonjwa wa COVID-19 katika baadhi ya mataifa duniani ambayo pia yana mwingiliano mkubwa wa kibashara na kijamii na Tanzania.

Katika kuhakikisha kuwa tunadhibiti ueneaji wa maambukizi haya, Serikali imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali ya wasafiri wanaoingia nchini kwa lengo la kudhibiti uingiaji wa anuai mpya ya virusi vya ugonjwa wa COVID-19.

Katika kutekeleza hilo, tarehe 04/05/2021 Serikali ilitoa mwongozo wa ushauri kwa wasafiri namba 7 (*Travel Advisory Note*) ambao unawataka wasafiri wote wanaoingia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka nchi yeyote duniani kufanyiwa uchunguzi wa kina wa afya zao na kuwasilisha cheti cha 'Real Time Reverse Transcription Polymerase Chain Reaction (RT-PCR)' vinavyothibitisha kuwa hawana maambukizi ya virusi (NEGATIVE) vya COVID-19 kutoka katika nchi wanakotokea.

Kutokana na mwenendo wa ugonjwa huu duniani na uibukaji wa anuai mpya ya virusi vya COVID-19 katika baadhi ya nchi na kwa kuzingatia namna ambavyo ugonjwa huu unaambukiza Wizara, ilielekeza wasafiri wote toka nje ya nchi wafanyiwe kipimo cha haraka (*COVID-19 Rapid Antigen Test*) cha ugonjwa wa COVID-19 pindi waingiapo nchini kupitia Mipakani, Viwanja vya Ndege vya Kimataifa na Bandari. Upimaji huu wa haraka (*COVID-19 Rapid Antigen Test*) unafanyika pia katika nchi nyingine duniani na kulipiwa zikiwemo nchi jirani, hivyo siyo Tanzania pekee.

Aidha, katika nchi mbalimbali, upimaji wa *COVID-19 Rapid Antigen Test* tayari umeweza kubaini wasafiri kadhaa ambao ni '*POSITIVE*' na walifika na vyeti vya RT-PCR

**NEGATIVE.** Gharama ya uchangiaji wa kipimo hiki cha haraka kwa Tanzania ni **dola za kimarekani 25 kila abiria**.

Wananchi wote na abiria wanaeleweshwa kuwa kipimo hiki ni muhimu kupimwa tena hata kama umepimwa siku chache zilizopita ili kujiridhisha na hali ya maambukizi, hasa yale yaliyotokea baada ya muda mfupi kabla au wakati wa kusafiri.

Hata hivyo, Serikali imepocha maoni ya abiria mbalimbali kuhusu uboreshaji wa ulipaji na upimaji wa **COVID-19 Rapid Test** katika viwanja vya ndege hasa katika kupunguza muda wa mlolongo wa upimaji. Kufuatia maoni haya, maboresho yamefanyika kwa kuongeza sehemu za kutolea huduma ikiwemo vituo vya kupima (kutoka 2 hadi 10), ulipaji kwa njia za kielektroniki (*kwa bank*) ili kupunguza muda kwa wasafiri kusubiria kufanya malipo. Hivi sasa mteja anatumia wastani wa dakika 15 kukamilisha mtiririko wa malipo na utoaji wa elimu kwa wasafiri juu ya kinga dhidi ya COVID-19. Tunawashukuru wananchi wote ambao wametoa ushauri wa kuboresha huduma hizi.

Kuhusu gharama za kipimo cha RT-PCR, kwa abiria wanaokuja Tanzania toka nje ya nchi ni kuwa, abiria hao hutakiwa kupimwa na kulipia katika nchi yake anakotokea yaani kabla hajasafiri na hii ni mojawapo ya sharti la ndege anayopanda. Hivyo, msafiri hutakiwa kuja kuonyesha cheti cha kipimo hicho katika viwanja vyote vya ndege vya kimataifa. Kwa hiyo gharama hizo za RT-PCR siyo mapato ya Serikali ya Tanzania. Kwa umuhimu huo, wasafiri wanakumbushwa kufuatilia na kuzingatia matakwa ya nchi wanakokwenda na mashirika ya ndege watakayotumia kusafiri kabla ya kuondoka nchini kwani baadhi ya mashirika ya ndege yanawataka kufanya kipimo kabla ya kusafiri.

Kwa wale wasafiri wanaolazimika kupima RT-PCR hapa nchini wanapotaka kwenda nje ya nchi, gharama kwa sasa ni dola za kimarekani 100 na fedha hizi ni za uchangiaji wa huduma ya vipimo kwani gharama halisi ni kubwa zaidi na Serikali ya Tanzania imekuwa ikibeba sehemu kubwa ya gharama husika.

Mwisho, Wizara inakumbusha kuwa lengo la upimaji wa abiria ni kuilinda nchi yetu na Jamii kwa ujumla dhidi ya maambukizi ya Virusi vya COVID-19. Hivyo, wasafiri wote wanashauriwa kuzingatia utaratibu huu pindi wanapoingia nchini na kutoa ushirikiano kwa wahudumu wetu uwanjani.

**Imetolewa na:**



Prof. Abel N. Makubi  
**KATIBU MKUU –AFYA**